

Tarehe 11.10.2023, Maafisa kutoka Ofisi ya Ustawi wa Jamii na Ofisi ya Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Morogoro wameshiriki katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kike Duniani, yaliyoandaliwa na Taasisi Isiyo ya Kiserikali ya C-Sema kwa kushirikiana na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), na kituo cha Amani Girls Home.



Akiwa miongoni mwa watoa mada katika maadhimisho hayo, Afisa Ustawi wa Jamii Manispaa ya Morogoro, Bi. Sidina Mathias amelishukuru kanisa la KKKT kupitia kituo chake cha Makimbilio kwa kuunga mkono jitihada za Serikali za kutoa ulinzi kwa mtoto ambapo amesema kituo hicho kimekuwa ni nyumba salama kwa watoto wengi ambao kesi zao huletwa kwenye Ofisi yake ya Ustawi wa Jamii.



“Uwepo wa Kituo cha makimbilio ambacho wengi hukiita Nyumba Salama, umetupa ahueni Maafisa Ustawi kuweza kujua kwamba wapi mtoto tunampeleka” alieleza Bi. SidIna.

Vilevile, Bi. SidIna ametoa wito kwa jamii kutosita kuwasiliana na Maafisa Ustawi walioko kwenye maeneo yao endapo kutakuwa na tukio lo lote la ukatili kwa mtoto au watoto kwa kuwa Maafisa Ustawi ndio ambao Sheria ya Nchi inawatambua kama walinzi wa Sheria ya Mtoto nchini.



Kwa upande wake Sheikh Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, ndugu Twaha Kilango, ambaye ndiye aliyekuwa mgeni rasmi katika maadhimisho hayo, ametoa wito kwa jamii kushikamana na kushirikiana kupaza sauti kutetea usalama wa watoto na kuhakikisha wanapata haki zao.

Pia, Sheikh Kilango ameitaka jamii itambue kwamba zama tulizonazo sasa ni zama za kusema mambo kwa uwazi bila kuyafumbafumba kwa sababu hata watoto wa sasa wanajua mambo mengi tu yanayotendeka duniani.



Naye Mratibu wa mradi wa Hapana Marefu Yasiyo na Mwisho, unaotekelezwa na Taasisi ya C-Sema, Bi. Patricia Mwaikenda, amesema mradi wa Hapana Marefu Yasiyo na Mwisho umelenga kuleta mabadiliko chanya ya mila na desturi potofu katika nchi yetu, ambazo kwa muda mrefu zimezuia ama kuchangia ukandamizaji wa kijinsia kwa wanawake, vijana na watoto. Miongoni mwa mila na desturi hizo ni pamoja na ndoa za utotoni ambazo wahanga wake wakubwa ni watoto wa kike.



Aidha, maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kike Duniani yalihudhuriwa na baadhi ya viongozi wa Dini za Kiislamu na Kikristo, Maafisa kutoka Manispaa ya Morogoro, wanafunzi wa baadhi ya shule za msingi na sekondari zilizopo Morogoro na wanawake machampioni wa mabadiliko kutoka Kata ya Mwembesongo.



MWISHO